

KILOMERO VALLEY TEAK COMPANY LIMITED
SERA YA AFYA NA USALAMA KAZINI

TOLEO LA JUNI, 2024



Utangulizi

KVTC inatambua kuwa maendeleo na shughuli zake, ambazo moja kwa moja ni za kiwanda cha misitu na uchakataji wa mbao, zinaweza kuwa na madhara katika Afya na Usalama wa wafanyakazi, wakandarasi na wageni wake. Kampuni itasimamia uendeshaji wake katika namna ya kupunguza hatari za Afya na Usalama.

Kampuni itafikia na kuendeleza sera hii kwa kuendelea kupima viwango vya ajali na matukio na kwa kubainisha hatari na fursa za uboreshaji endelevu unaohusiana na hatari hizi utaanzishwa. Shughuli za kampuni zitajumuisha kiwanda cha kuchakata mbao, utunzaji mashamba ya miti, bustani ya miti, uvunaji wa miti na usafirishaji.

Kampuni itaendeshwa na kufuatilia utendaji wake kulingana na misingi ifuatayo:-

Sera

1. KVTC itafuata sheria na kanuni zote zinazohusu Afya na Usalama wa wafanyakazi na familia zao. Pia itafuata viwango vya ISO 45001:2018, Miongozo ya Kiwanda ya IFC na misingi inayohusiana na Afya na Usalama ya FSC.
 - a. Miongozo ya Afya na Usalama itapatikana kwa waajiriwa wote wa kampuni.
 - b. Menejimenti ya kampuni na wote walioajiriwa na kampuni watafahamu maudhui ya miongozo ya Afya na Usalama na kampuni.
 - c. Kampuni na wale wote iliyowaajiri watatathimini hatari kwa wafanyakazi kulingana na kazi na vifaa na kuchukua hatua zinazostahili kwa lengo la kupunguza au kuondoa hatari hizo.
 - d. Mafunzo ya usalama yatafanyika, kufuatana na kazi za wafanyakazi na vifaa vinavyotumika kama ilivyoeleza katika sheria.
 - e. Wafanyakazi watapatiwa vifaa vya usalama vinavyohusiana na kazi za wafanyakazi na vifaa vinavyotumika, kama inavyoonyeshwa katika taratibu za kampuni.
 - f. Kampuni itachukua hatua zinazostahili kuhakikisha matumizi ya vifaa vya usalama kwa wafanyakazi na wakandarasi wake kama ilivyooonyeshwa katika taratibu za kampuni.
 - g. Kampuni itaweka kumbukumbu ya ajali na vifo vyote vinavyohusiana na kazi za wafanyakazi, sababu za kutokea, na kuweka kumbukumbu ya hatua zilizochukuliwa kuzuia ajali kama hizo sizitokee siku zijazo, na kutekeleza hatua hizo za uzuiaji.
 - h. Kampuni itaainisha mahitaji ya wadau husika na changamoto za ndani na nje ya Kampuni zinazoathiri ufanisi wa afya na usalama kazini na kuzifanyia kazi kulingana na taratibu za Kampuni.
2. KVTC itachukua hatua zinazostahili kuboresha kiwango cha jumla cha afya na huduma za jamii katika jamii zinazohusiana moja kwa moja na KVTC.
 - a. Kampuni itasaidia programu za elimu kwa jamii zinazolenga kwenye masuala ya msingi na muhimu ya uangalizi wa afya.
 - b. Kampuni itashiriki katika maendeleo yanayofaa ya kiuchumi ili kusaidia na kufanikisha miradi endelevu ya kujisajdia.

Irvine Kanyemba Mkurugenzi Mtendaji